SEHEMU YA KWANZA

MBONA KITABU CHA MAELEKEZO YA MAFUNZO KWA SALA YA UINJILISTI KWA MWAKA 2000?

LENGO: KUWAFUNDISHA NA KUWATAYARISHA WANAWAKE NA WANAUME ULIMWENGUNI, WA MADHEHEBU, MASHIRIKA YA MAKANISA YOTE KUWAOMBEA NA KUWAFIKIA WALE AMBAO HAWAJAFIKIWA NA NENO LA YESU KRISTO.

Watu wasiopungua bilioni mbili ulimwenguni leo, kamwe hawajasikia ushuhuda wazi kuhusu Habari Njema, kwamba Yesu Kristo alikufa kuwaokoa kutoka dhambi zao! Wakristo watafanya nini kuhusu jambo hili? Tujali vya kutosha ili tuweze kuchukua hatua? Lengo la kitabu hiki ni kuwasaidia wanawake kwa wanaume ulimwenguni kuyajibu maswali haya na kufanya kazi kupitia sala na kueneza injili ili kuwafikia mabilioni ya wale ambao hawajalisikia neno la Mungu.

1. MBONA TUUARIFU ULIMWENGU MZIMA KUHUSU YESU?

A. Lazima tutii amri ya Yesu kwamba twende tukawafanye watu wa mataifa yote wawe wafuasi. Matayo 28: 18 - 20. (Soma Mariko 16: 15 na Luka 24: 46-47)

B. Agizo la mwisho kwa wafuasi wake lilikuwa, tuwe mashahidi wake hata katika MIPAKA YA DUNIA. Matendo 1:8.

C. Mungu awataka watu wote waokolewe na wapate kujua ukweli. 1 Timotheo 2:4 (Soma II Petero 3:9 (na Tito 2:11)

D. Yesu alilipa yeye binafsi, sio tu kwa dhambi zetu, bali kwa dhambi za ulimwengu mzima.

E. YESU ALITEKELEZA WAJIBU WAKE MSALABANI: LAKINI HAKUFANYA, NA HANGEWEZA KUFANYA YALE ALIYOTUACHIA TUYAFANYE - KUUFIKISHIA ULIMWENGU UJUMBE WAKE WA WOKOVU. (Alimfikia mtu mmoja tu, mwizi aliyekuwa akifa msalabani.)

F. Yesu yuwarudi, lakini mwisho hauwezi kufika hadi injili ya ufalme wa Mungu itakapohubiriwa kote.

"Na injili ya Ufalme itahubiriwa ulimwenguni kote kama ushuhuda kwa mataifa yote, na kisha mwisho utafika." Matayo 24:14.

1. Ufunuo 7:9-10 watuambia kwamba ushindi wa mwisho utawashirikisha watu kutoka kila taifa, kabila, na lugha duniani. (Soma Ufunuo 5:8-9)
2. Hakupasi kuwepo na vizuizi zaidi kwa uelewano au kukubaliwa kwa injili kutokana na utamaduni, lugha au maumbile ya dunia ambayo habari njema za Yesu hazijavuka kabla ya mwisho kufika.

II JE, BIBLIA KWELI HUSEMA KWAMBA WATU WOTE AMBAO HAWAJAMKUBALI YESU, HATA KUTOKA DINI NYINGINE WAHITAJI KUENEZEWA INJILI?

A. Kila mmoja AMEHUKUMIWA NA KUPOTEA hadi amkubali Yesu.
   1. Yesu asema katika Yohana 3:18 kwamba wote wamehukumiwa tayari, isipokuwa wamwamini.
   2. Kupitia dhambi moja (ya Adam na Eva) kulitokea hukumu kwa watu wote (Warumi 5: 18)

B. Watu wote wahitaji DHAMBI ZAO ZISAMEHEWE kupitia uokovu.
   1. Watu wote ulimwenguni wangali katika ile hali ya dhambi ya kwanza ambamo walizaliwa, hadi watakapookoka (Warumi 5:18-19, na Luka 24:46-47)
   2. *"Watu wote wametenda dhambi na wamepungukiwa na utukufu wa Mungu."* (Warumi 3:23.)

C. Zipo falme mbili tu za kiroho - Ufalme wa Yesu na wa Shetani, na watu wote duniani wamo katika mojawapo ya falme hizo.
   1. Ufalme wa shetani ni wa GIZA na ule wa Yesu ni wa NURU. (Wakolosai 1:13 na Matendo 26:18)
   2. "*Twajua kwamba sisi* (wakristo) *ni wake Mungu, ingawa ulimwengu wote* (usio wa Yesu) *watawaliwa na mwovu.*" 1Yohana 5:9.

D. Uokovu huwahamisha watu kutoka ufalme wa shetani hadi ufalme wa Yesu.
   "Yeye alituokoa kutoka nguvu za giza, na akatuhamishia Ufalme wa mwanawe mpendwa." Wakolosai 1:13.

   "Mimi ni mwanga, nami nimekuja ulimwenguni ili wote wanaoniamini wasibaki gizani. Yohana 12:46.

   1. Yesu alimwambia Paulo katika barabara ya Damaska kwamba madhumuni ya kumwita yalikuwa "kuyafungua macho yao ili waweze kuondoka gizani na kuingia katika mwanga, na waondoke kutoka utawala wa shetani na wamgeukie Mungu." Matendo 26:16-18
   2. Kueneza injili ni vita vya kiroho, huku wakristo wakishiriki na Yesu katika mapambano kati ya watawala wa falme hizo mbili za ulimwengu ya kung'ang'ania roho za wapotevu duniani.
      a. Shetani anajaribu kushikilia wale ambao tayari ni wake, kwa sababu walizaliwa wakiwa tayari wamehukumiwa katika UFALME WAKE WA GIZA.
      b. Yesu yu-watuita tusaidie kuwaokoa wale ambao wangali utumwani katika ufalme wa shetani - ili Mungu awahamishe hadi ufalme wa Yesu.

III WASIOMKUBALI YESU WATAKUWAJE?

A. Wote wasiomwamini Yesu wataishi maisha yao ya milele katika jahanamu.
   "Na ikiwa jina la mtu ye yote halikupatikana limeandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika ziwa la moto." Ufunuo 20:15

B. Je, Biblia husema jahanamu ni nini?
   1. Kigriki = Ghenna. Lilitumiwa na Yesu mara 11 kati ya mara 12 linapopatikana katika agano jipya. (Matayo 20:28).
   2. Wakazi wa jahanamu wako katika hali mbili:
      a. Ibilisi na malaika wake - watu wasio wa kawaida (Ufunuo 20:10).
      b. Watu waliolaaniwa - binadamu (Matayo 25:41; na Ufunuo 20:15).
   3. Maelezo ya makao ya milele ya wasiookoka.
      a. Mahali ambapo huwezi kutoroka. (Matayo 23:33)
      b. Mahahi pa moto. (Matayo 13:49-50)
      c. Mahali pa mateso. (Matayo 13:50)
      d. Mahali pa adhabu, sio pa marekebisho. (2 Watesalonike 1:8)
      e. Mahali pa waliohamishwa na kutengwa (2 Watesalonike 1:9; na Matayo 7:23)
      f. Mahali pa milele (Mariko 9:47-48; Ufunuo 14:11)
         Katika matayo 25:46, Yesu alitumia neno hilo 'milele' kwa muda wa adhabu kama alivyotumia neno hilo kwa 'maisha ya milele kwa wanaoamini."

IV. MUNGU ALIWAPANGIAJE WALE WALIOPOTELEA KATIKA UFALME WA SHETANI?

A. Mungu aliwapenda watu duniani vya kutosha kutoa dhabihu kuu ya mwanawe Yesu kwetu.
   "Maana Mungu aliupenda ulimwengu, hivi hata akamtoa mwanawe wa pekee, ili kila

anayemwamini asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16.

B. *"Lakini Mungu hudhihirisha upendo wake kwetu, hivi kwamba tulipokuwa bado tu wenye dhambi, Kristo alitufia."* Waroma 5:8.

C. *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni kifo, lakini zawadi ya bure anayoitoa Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.* Waroma 6:23.

D. *Kristo hakuwa na dhambi, lakini Mungu alimfanya ahusike na dhambi kwa ajili yetu, ili sisi kwa kuungana naye, tupate kuushiriki uadilifu wake Mungu."* 2 Wakorinto 5:21.

E. Lakini Yesu alimshinda shetani msalabani.
"Akaonekana kama mwanadamu, alijinyenyekeza na kutii mpaka kufa, hata kufa msalabani, Kwa sababu hiyo, Mungu alimkweza juu kabisa, akampa jina lililo kuu zaidi kuliko majina yote. Ili kwa heshima ya jina la Yesu, viumbe vyote mbinguni, duniani na kuzimu vipige magoti mbele yake, na kila mtu akiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba. Wafilipi 2:8-11

F. Na Yesu akasema, *'Ye yote anayemwamini Mwana, anao uzima wa milele, lakini asiyemtii Mwana, hatakuwa na uzima wa milele, bali hasira ya Mungu hubaki juu yake.* Yohana 3: 36.

V. NINI HUTOKEA MTU ANAPOMKUBALI YESU KUWA MWOKOZI NA BWANA?

A. Twazaliwa upya.
"Kweli nakuambia, mtu asipozaliwa upya, hataweza huuona ufalme wa Mungu. Yohana 3:3.

B. Twahamishwa kutoka utawala wa shetani hadi ufalme wa Mungu.
1. Wakolosai 1:13, na Matendo 26:14-18.
2. *'Nimekuja kama Mwanga ulimwenguni ili wote wanaoniamini wasibaki gizani."* Yohana 12:46.

C. Dhambi zetu zimesamehewa.
1. *"Manabii wote waliongea juu yake kwamba kila mtu atakayemwamini atasamehewa dhambi zake kwa jina lake.* Matendo 10:43.
2. *"Yesu Kristo alitukomboa kutoka dhambi kwa damu yake."* Ufunuo 1:5.
3. *Maana kwa damu yake Kristo, sisi tumekombolewa, Ndivyo Ukuu wa neema yake.* Waefeso 1:7.
4. Soma Wakolosai 1:13 - 14 na Matendo 26:18.

D. Tumefanywa kuwa na uhusiano mwema na Mungu kwa kifo cha Kristo, na kutuepusha kutokana na ghadhabu ya Mungu. (Waroma 5:9)

E. Waaminio wamo ndani ya Kristo, na Kristo yu ndani yao. (Yohana 14:20)

F Tu viumbe vipya katika yesu (2 Wakorinto 5:17)

G. Tunao uzima kamili katika Yesu. (Yohana 10:10)

H. Tunapokea uzima wa milele (Yohana 3:16)

I. Tunao uridhi mbinguni (1 Petero 1:3-4; Matendo 26:18)

J. Mungu hupokea neema yote kutokana na uokovu wetu. (Wagalatia 1:3 - 5)

VI. MTU LAZIMA AFANYE NINI ILI KUMKUBALI YESU?

A. Mwamini Yesu aliyekuja akihubiri akisema katika Mariko 1:15 "Tubuni na mwamini"
B. Akubali kwamba yeye ni mwenye dhambi. (Matendo 2:38)
C. Amwamini Yesu. (Yohana 3:16)

VII. ULIMWENGU UTAPATAJE HABARI NJEMA TUSIPOUAMBIA ?

A. Yesu alitekeleza wajibu wake msalabani; lakini hakuweza, na hangeweza kueneza injili akiwa msalabani.
B. Yesu alituachia wajibu wa kueneza ujumbe wa uokovu wake katika ulimwengu wote.

"Ye yote atakayeomba kwa jina la Bwana, ataokolewa. Basi watu watamwombaje yeye ambaye hawamwamini? Na watamwaminije ikiwa hawajahubiriwa? Na watasikiaje habari zake kama hakuna mhubiri? Na watahubiriwaje kama hawakutumwa?"
Waroma 10:13-15.

MAZOEZI

Chunguza moyo wako. Unayo sababu gani kudai wewe ni mkristo? Umewahi kumkubali Yesu kwa kutubu dhambi zako na kumwamini, ukimruhusu Mungu kukuhamisha kutoka utawala wa shetani hadi ufalme wake? Ikiwa hujafanya hivyo, fanya sasa. SEHEMU YA KITABU HIKI ILIYOBAKI HAITAKUHUSU HADI UFANYE HIVYO.

Chunguza kila sababu ambayo umetoa kwa kutosali na kutowahubiria wapotevu kwa niaba ya Yesu.

* Sikujua mafundisho ya Biblia kwamba wote wamepotea hadi watakapomwamini Yesu.
* Sikufahamu ukweli na tisho ya jahanamu kwa wasiookoka.
* Sijakubali wajibu wangu wa kutii amri ya Yesu katika utenzi wake mkuu.
* Nimekuwa nikishughulika na kuitunza jamaa yangu na mimi mwenyewe na sikuweza kujali kuhusu shida za watu wengine.
* Kanisa na shirika langu la kikristo huona uenezi wa injili kama mradi tu - si kuokoa roho kutoka utawala wa shetani.
* Nimefundishwa kuzivumilia dini za watu wengine, na kwamba nisifikirie yangu kuwa bora kuliko zao.
* Kwa kuwa Mungu yuwajua wale watakaookoka, sina haja kujali.
* Nakosa uwezo wa Roho mtakatifu wa kutumia na kubariki juhudi zangu hafifu.
* Naogopa kutofaulu.
* Naogopa kujadili mambo ya kiroho.
* Afadhali nipendwe na watu, badala ya kuilazimisha dini yangu kwao.
* Sijajali

SALA YAKO

1. Mwombe Mungu akusamehe kwa kila sababu umetoa kwa kutojali kuwaombea na kuwaleta watu kwa Yesu.
2. Mwombe Mungu akupe wajibu wa kuwapashia injili wale walioko karibu nawe, na kote ulimwenguni.
3. Mwahidi Mungu kwamba utaanza kuwaombea kwa uaminifu wale wapotevu.
4. Mwahidi Mungu kwamba utatii atakapokuagiza kuwashuhudia waliopotea.

Kwa mafunzo kamili kuhusu swala hili, soma kitabu kiitwacho 'Kupigana vita na mwana-mfalme wa Giza.